## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2012 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2009, 2010 na 2011.

***Jedwali 7: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2009 hadi 2012***

| | 2009 | | 2010 | | 2011 | | 2012 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 28.65 | 21.48 | 26.38 | 20.12 | 20.77 | 21.89 | 23.37 | 21.99 |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 30 | 20 | 27 | 20 | 20 | 20 | 24 | 20 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 50 | 40 | 49 | 39 | 47 | 40 | 48 | 39 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

a) Alama ya wastani ilipanda kutoka **20.77** mwaka wa 2011 hadi **23.37** mwaka wa 2012.

b) Alama ya juu iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2012 ni **48** tofauti na **47** ya mwaka wa 2011.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **24** tofauti na **20** ya 2011.

d) Alama ya wastani katika karatasi hii inaanza kuimarika tangu ilipoanza kushuka mwaka baada ya mwaka kuanzia 2009.

**Katika Insha:**

a) Alama ya wastani ilipanda kutoka **21. 89** ya mwaka wa 2011 hadi **21.99** mwaka wa 2012.

b) Alama ya juu zaidi iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2012 ni **39** tofauti na **40** ya mwaka wa 2011.


c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20** kama iliyyokuwa mwaka 2011.

d) Alama wastani inaelekea kufikia kiwango kinachokubaliwa ( **20/40**) japo imepita kiwango hiki kiasi.



Powered by: www.manyamfranchise.com


Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.




### 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

#### 4.1.1 Uchanganuzi wa maswali maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali:




#### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa

Katika mwaka wa 2012, yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini (30%). Maswali yafuatayo ndiyo yanayochukuliwa kuwa yaliwatatiza wanafunzi zaidi: Swali 1, 4, 7, 33, 34, 38 na 43.

***Jedwali 8: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa***

| *Maswali* | *1* | *4* | *7* | *33* | *34* | *38* | *43* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi* | *17.87* | *21.78* | *19.73* | *20.76* | *10.16* | *13.97* | *16.10* |
| *Asilimia ya wastani ya mswali yale mengine* | *25.81* | *26.39* | *26.86* | *26.24* | *23.52* | *23.91* | *25.10* |



Powered by: www.manyamfranchise.com

### 4.1.3 Ruwaza za majibu

**Maswali 1 mpaka 15**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Kiswahili ni mojawapo ya lugha _1_ wazungumzaji wengi. Lugha ya Kiswahili _2_ zama za ukoloni _3_ Waafrika dhidi ya wakoloni.

Hatua ya kukifanya Kiswahili lugha rasmi nchini Kenya _4_ hadhi ya lugha husika. _5_ hapo awali, tunatarajia Kiswahili kutumiwa _6_ na Kiingereza katika shughuli za kiofisi. Hata hivyo, _7_ ; patakuwa na haja ya kutafsiriwa kwa makala mengi kwa Kiswahili.

**Swali la 1**

A. yenye B. zenye C. wenye D. chenye

**Matokeo ya swali la 1**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 72.97 | 17.87 | 5.27 | 2.67 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23.30 | 25.81 | 18.14 | 20.63 |

Swali hili lilitahini upatanisho wa kisarufi katika hali ya wingi. Dhana ya wingi ilidokezwa na neno, 'mojawapo', linalomaanisha,' miongoni mwa'.Hata hivyo, watahiniwa wengi, kwa kuona neno lugha, walifasiri kwamba ni neno hilo tu ambalo linapatanishwa na maneno mengine katika sentensi. Walipuuza neno, 'mojawapo' ambalo liliwaelekeza kufahamu kwamba Kiswahili ni lugha moja tu kati ya nyingine nyingi.Ni muhimu kwa walimu kufunza dhana hii.

**Swali la 4**

A. imeieneza B. imeitia fora C. imeikweza D. imeivika kilemba

**Matokeo ya swali la 4**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 31.51 | 34.15 | 21.78 | 11.25 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23.47 | 21.79 | 26.39 | 22.40 |

Swali hili lilitathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuoanisha maneno katika msururu wa kauli na kuyaunganisha kimantiki kuibua wazo kamili.
Watahiniwa wengi walichagua jibu **B :imeitia fora** bila kuzingatia vipashio vingine jirani. Kutia fora ni nahau inayomaanisha kuwa bora. Mtu hawezi kuitia fora hadhi.


Powered by: www.manyamfranchise.com

**Swali la 7**

A. hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe B. hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
C. hakuna bamvua lisilo usubi D. hakuna kubwa lisoshindwa

**Matokeo ya swali la 7**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 39.40 | 28.09 | 19.73 | 11.45 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 22.13 | 22.86 | 26.86 | 23.26 |

Swali hili lilitahini stadi ya usanisi.Mtahiniwa alihitajika kujumuisha ujumbe wa maneno ya awali kwa kutumia methali.Asilimia kubwa ya watahiniwa iliteua jibu **A**.Yaelekea kwamba watahiniwa hawa walivutiwa zaidi na methali hiyo kwani ndiyo inayoelekea kuzoeleka sana na watahiniwa. Ni muhimu watahiniwa kusoma viteuliwa vyote na kupima uhusiano wake na kauli za awali au maneno jirani ili kufikia jibu sahihi.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Kuna aina mbili kuu za misitu. Ipo ile ya kiasili kama vile Msitu wa Karura na Msitu wa Mau. Hali kadhalika, ipo misitu ya kupandwa kama ile ya Kinale na Webuye. Misitu ni hazina kubwa kwa jamii yoyote ile. Kila mwanajamii anapaswa kujivunia misitu.

Misitu husheheni miti ya aina nyingi ambayo, pamoja na kuwa makazi ya wanyama, hutoa vyakula kama vile matunda na majani ambayo huwafaidi binadamu na viumbe wengine. Bila misitu binadamu na wanyama wangeangamia.

Misitu ni kivutio cha watalii. Watalii kutoka ndani na nje ya nchi huzuru misitu na mbuga mbalimbali za wanyama kuajabia uzuri wake. Watalii hawa hulipa fedha za kigeni ambazo hutumiwa kuanzishia miradi ya kiuchumi kama vile kustawisha miundomsingi.

Fauka ya hayo, misitu husafisha hewa na kurembesha mandhari wanamoishi binadamu. Rangi ya kijani kibichi na maua yenye rangi tofautitofauti huyafanya mazingira kupendeza hata yakitazamwa kwa mbali. Mandhari yasiyo na miti hayakosi urembo tu, bali huwa wazi kiasi kwamba hata mapaa ya majengo yaliyo hapo wakati mwingine hupeperushwa na upepo mkali.

Vipindi virefu vya jua huwanyima viumbe starehe na huweza kusababisha saratani ya ngozi kwa binadamu. Miti hufanya vivuli ambavyo huwakinga watu na wanyama dhidi ya miale ya jua. Isitoshe, si ajabu kuwa mahali ambapo pana miti mingi kwa kawaida hupata mvua hata wakati usio wa majira ya mvua kwingineko.

Sekta ya tiba imefaidika si haba kutokana na miti. Matabibu wa kienyeji na hata wa kisasa hutumia mizizi, majani na magome ya miti kutengenezea dawa. Miti kama vile mwarubaini hutibu magonjwa mengi. Hivi sasa magonjwa kama vile bolisukari, shinikizo la damu na ugonjwa wa figo yameweza kudhibitiwa kwa kutumia dawa zinazotokana na miti. Inasemekana kuwa hata nyoka humtibu nyoka mwenzake kwa majani!

Miti hutumiwa viwandani kutengenezea bidhaa kama vile karatasi na samani. Viwanda hivi hutoa ajira kwa maelfu ya raia, hivyo kupunguza makali ya uhaba wa nafasi za kazi nchini.


Powered by: www.manyamfranchise.com

Ni wazi kuwa uhifadhi wa misitu una manufaa tumbi nzima kwa binadamu. Hata hivyo, binadamu mwenyewe ndiye anayeiangamiza misitu yenyewe. Watu wenye mate ya fisi wamekata miti kiholela kwa ajili ya kupata kuni na kuchomea makaa ya kuuza. La kusikitisha ni kwamba watu hawa **hawadiriki** kupanda miti mingine kufidia ile waliyoikata. Wengine, kwa kutojua wanajipalia makaa, hupanda miti ambayo inakausha vyanzo vya maji na kuchangia kuenea kwa kasi kwa jangwa. Hali kadhalika, wapo warina asali ambao katika juhudi zao za kurina husababisha kuteketea kwa misitu.

Kifungu cha katiba kinachohusu mazingira na mali ya asili kinasisitiza suala la uhifadhi wa mazingira. Kila mwanajamii basi ana jukumu la kuilinda misitu na kuepuka mazoea ambayo yanaiangamiza, la sivyo tutakuwa tunajichimbia kaburi.

**Swali la 33**

Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?
A. Dawa za kienyeji huponya kabisa magonjwa mengi sugu.
B. Kuhifadhi misitu kunaweza kuchangia kubongezeka kwa nafasi za kazi.
C. Mahali penye miti mingi hupata mvua inayotegemewa kila mara.
D. Kuwa na vipindi virefu vya jua kali kunaweza kusababisha saratani.

**Matokeo ya swali la 33**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 13.35 | 20.76 | 24.63 | 39.78 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.10 | 26.24 | 21.66 | 23.81 |

Hili ni swali la kiutekelezaji .Mtahiniwa alihitajika kutumia ujuzi wa yaliyomo katika taarifa kuteua jibu sahihi. Watahiniwa wengi waliteua jibu **D**, pengine kwa kuwa kifungu kinataja nafasi ya vipindi vya jua katika kusababisha saratani.Hata hivyo taarifa inazungumzia vipindi virefu, wala si ukali wa jua tu. Linalojitokeza hapa ni kwamba wanafunzi wengi hawadiriki kusoma vifungu kwa makini.

**Swali la 34**

Kifungu kinasema kuwa miti hutumiwa:
A. kutengenezea kawi na kuwasetiri viumbe;
B. kuunda samani na kuhifadhi maji;
C. kusafishia hewa na kufanikisha majengo;
D. kuvuta mvua na kuburudisha viumbe.

**Matokeo ya swali la 34**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 10.16 | 28.43 | 26.67 | 33.26 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23.52 | 23.37 | 23.15 | 23.64 |

Swali hili lilitahini stadi ya matumizi.Mtahiniwa alihitajika kutumia ufahamu wake wa yaliyomo katika kifungu kujibu swali. Hata hivyo, asilimia kubwa ya watahiniwa ilichagua jibu **D**, pengine kwa kuathiriwa na maarifa yao katika somo la Sayansi. Watahiniwa hawakuzingatia kwamba kimantiki miti haiwezi kuburudisha.Ni muhimu walimu kuwazoesha wanafunzi wao kujibu aina hii ya maswali.

Powered by: www.manyamfranchise.com

**Swali la 38**

Kulingana na aya ya mwisho:
A. Mazingira huhifadhiwa kupitia kwa kifungu cha katiba.
B. Mwanajamii hujiletea majuto kwa kutoepuka mienendo isiyokubalika.
C. Mazingira huharibiwa na hulka zisizofaa za binadamu.
D. Mwanajamii anastahili kufuata mshawasha wa katiba.

**Matokeo ya swali la 38**

| **Majibu** | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 26.57 | 23.83 | 13.97 | 34.18 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.52 | 23.84 | 23.91 | 24.39 |

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kujumuisha ujumbe wa aya ya mwisho. Hata hivyo wengi walishindwa kung'amua kwamba walihitajika kutumia stadi ya utekezaji wala si ukariri.Walivutiwa na neno,'katiba' na wengi wao kuteua jibu **D**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Tenga alilelewa katika mazingira yaliyojaa neema, furaha na uchangamfu. Wazazi wake Bwana Mtanga na Bi. Zuhura walikuwa wakwasi wa kutajika katika janibu hizo, si kwa mali tu bali kwa nyoyo zao zilizokuwa tayari kila mara kuwakirimu wanakijiji kwa lolote.

Bwana Mtanga na Bi. Zuhura hawakulala maskini wakaamka matajiri. Mtanga alianza kazi kama tarishi katika Makavazi ya Umma. Ingawa hii ilikuwa kazi ya kijungu jiko mekoni, Mtanga **hakwenda nguu**; alijitahidi kwa vyovyote vile kujinyanyua. Akajisajili kwa kozi mbalimbali za usimamizi wa makavazi na kuhitimu vyeti tofautitofauti vikiwemo stashahada na shahada katika masuala ya usimamizi wa mashirika ya umma. Jitihada zake zikazaa matunda. Akapandishwa cheo mwaka baada ya mwingine hadi akawa msimamizi wa Makavazi ya Umma. Baadaye akaajiriwa na shirika la Msalaba Mwekundu kama Mkrurugenzi wa Huduma za Kijamii.

Bi. Zuhura naye, baada ya kuhitimu masomo ya shule ya upili, alisomea taaluma ya ukutubi na baadaye kuajiriwa katika maktaba ya chuo kikuu cha Tungama. Hapa Zuhura alitambua kuwa amepata nafasi adimu ya kuutia makali ubongo wake. Akajisajili kwa kozi ya ukutubi na kuhitimu shahada ya daraja la kwanza katika taaluma hii. Wakuu wake kazini wakavutiwa na juhudi zake na kumpandisha cheo, akawa Mkutubi Mkuu.

Wakati Bwana Mtanga na Bi. Zuhura walipokuwa wakijiendeleza kitaaluma na kiuchumi, Tenga naye alikuwa anajikulia tu kama uyoga bila mpalilizi. Nyadhifa za wazazi wake zilimpokonya Tenga ushirika wa wazazi wake. Ile michezo yake na wazazi wake kabla ya chajio, yale matembezi ya kila Jumapili ... yote yakatoweka. Baba na mama wakawa wanarudi nyumbani baada ya saa nne usiku wakiwa wametoka kwenye masomo ya kuupigia msasa ujuzi wao; Jumamosi na Jumapili wana majadiliano na wanafunzi wenzao. Nyakati nyingine wazazi wote wawili walikuwa kwenye safari za kikazi. Nyakati kama hizi Tenga angepelekwa kwa shangazi ambako angekaa na kijakazi wake kwa wiki tatu; anaenda shuleni na kurudi huko huko kwa shangazi.

Wahenga walisema kwamba, akosaye la mama hata la mbwa huamwa. Pengo la malezi lililoachwa na wazazi wa Tenga lilijazwa na walezi wengine, wakiwemo vijakazi, shangazi, marika, walimu, majirani na hata vibonzo! Tenga alijifunza mengi kutokana na walezi hawa. Alifunzwa namna ya kupigana



Powered by: www.manyamfranchise.com

miereka, kutumia ujanja kujitoa katika matatizo, kutumia maneno makali **kujihami** alipochokozwa na wenzake, pamoja na mitindo mbalimbali ya kujinadhifisha.

Mafunzo ambayo Tenga aliyapata, hasa kutoka kwa marika, yaliutia ila mwenendo na uhusiano wake na walimu. Darasani akawa haishi kuvuruga masomo kwani kila mara angetenda kituko ili mwalimu na wanafunzi waubaini uwepo wake. Vituko hivi vilisababisha kudorora kwa alama zake. Walimu wakajaribu kuurekebisha utundu wake lakini zikawa kama juhudi za mfa-maji. **Tabia ya Tenga haikuwa ufa tena bali ukuta ambao ulihitaji kujengwa upya**. Mkuu wa Idara ya Ushauri na Uelekezaji shuleni ilibidi ahusishwe. Akamhoji Tenga na kupambaukiwa kuwa vitendo vya Tenga vilikuwa na asili ambayo ilihitaji kuchunguzwa. Akampendekezea mwalimu wa darasa kuwashirikisha wazazi katika kutafuta mbinu za kumwelekeza Tenga zaidi.

Bwana Mtanga na mkewe Zuhura walipoambiwa kuhusu hali ya Tenga walipigwa na bumbuazi. Hawakuwa wameyawazia madhara ya kutoshiriki kikamilifu katika malezi ya mtoto wao. Mwalimu aliwaambia ya kwamba nusura Tenga aingizwe na wenzake katika matumizi ya dawa za kulevya lakini akakataa na kusema kuwa hata babake hakujaribu kutumia kileo chochote. Wazazi waliona haya na kujilaumu. Hata hivyo walishukuru ya kwamba walimu waliyagundua matatizo haya kabla hayajaiangamiza familia yao.

**Swali la 43**

. Wazo **kuu** linalojitokeza katika aya ya **nne** ni kwamba:

A. Jambo lolote likifanywa bila ushirikiano huweza kuleta madhara.
B. Jambo lolote likifanywa bila kipimo huweza kuleta madhara.
C. Jambo lolote likifanywa bila utulivu huweza kuleta madhara.
D. Jambo lolote likifanywa bila mtazamo huweza kuleta madhara.

**Matokeo ya swali la 43**

| **Majibu** | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 42.77 | 16.10 | 9.52 | 29.85 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 23.07 | 25.10 | 19.40 | 24.30 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kutathmini na kutoa uamuzi ufaao.Hata hivyo, watahiniwa wengi, pengine kwa kutokuwa makini, walikosa kuona kulikokuwa na kiini cha jibu.Wengi walikimbilia jibu **A** ambalo lilihusiana na ushirikiano wala si umuhimu wa kutenda mambo kwa kipimo.

Kwa jumla uchanganuzi wa mtihani wa mwaka 2012 umebainisha kwamba utendaji wa wanafunzi katika maswali ya ufahamu umeanza kuimarika. Asilimia kubwa haikutatizika na maswali ya ufahamu kama ambavyo ilikuwa kawaida katika mitihani ya miaka ya awali.

Kadhalika imebainika kwamba watahiniwa bado wanafanya vyema zaidi katika ufahamu wa kibunilizi ikilinganishwa na utendaji katika ufahamu wa kimaelezo.Ni muhimu walimu kuwaongoza wanafunzi zaidi katika kujibu maswali ya aina zote mbili za ufahamu.Pia wanafunzi wanastahili kuhimizwa kusoma kwa mapana ili kukukuza stadi za kukabiliana na maswali ya ufahamu wa kuandika.



Powered by: www.manyamfranchise.com

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

**Katika mwaka wa 2012 mada ya insha ilikuwa:**

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.**

Andika insha inayoanza kwa **maneno yafuatayo:**

***Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya.***

Swali hili lilitahini insha bunilizi za mdokezo. Mtahiniwa alihitajika kubuni kisa ambacho kinaafikiana na hali inayomkumba mhusika mwanzoni.

### a) Maudhui/yaliyomo

Hapa mtahiniwa alihitajika kusimulia kisa ambacho kinadhihirisha hali ya furaha na sababu za furaha hiyo. Masuala ambayo yalitarajiwa ni kama vile:

i) Mhusika au msimulizi amefaulu kuliko alivyotarajia katika mtihani.
ii) Msimulizi alikuwa katika hali ya hatari, akaponea chupuchupu.
iii) Msimulizi amekuwa amepotelewa na rafiki au jamaa kwa muda mrefu, hana matumaini ya kumwona lakini kwa bahati anatokea.
iv) Msimulizi ana rafiki au jamaa mgonjwa mahututi lakini ananusurika.
v) Msimulizi na wenzake wamo katika mashindano makali na timu nyingine ambayo ni bingwa na hatimaye wanaibuka washindi., n.k

### b) Muundo na mtindo

Muundo wa hadithi fupi ulihitajika. Yafuatayo yalitarajiwa kubainika:

**i)** **Mwanzo** unaoonyesha hali inayomfanya msimulizi kuwa na furaha.
**ii)** **Mwili** ambamo ndimo hasa kisa kinaposimuliwa na kukuzwa.
**iii)** **Uteuzi mwafaka** wa tamathali za lugha na mbinu nyingine za kimtindo zinazolenga kukuza mada husika
iv) Kuzingatia kaida za kisarufi
v) Maendelezo mwafaka ya maneno
vi) Kusimuliwa kwa kisa kwa hati nadhifu inayosomeka
**vii)** **Hitimisho** ambapo msimulizi anakamilisha kisa chake. Mwisho unaweza kuwa wa taharuki, akamwacha msomaji na hamu ya kutaka kujua lililotokea, au akaonyesha pia mustakabali wa maisha yake baada ya tukio hili.

### 4.2.1 Vigezo vya kutathminia

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa walivyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum, na mambo ambayo yanazingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40



Powered by: www.manyamfranchise.com

### 4.2.2 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)

Watahiniwa katika kitengo hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama **01-05** hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muwala na muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote, ama na msamiati finyu, au na mada husika. Udhaifu wao kimawasiliano huwakosesha kukuza mada/ maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama **06-10** hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Hata hivyo, insha zao huwa na mategu mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujieleza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka au kupungukiwa kimaudhui/upande wa mada na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili( huwa na athari nyingi za lugha ya mama).

**Mtungo wa kwanza**

**Ulipewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Sana Kama wiliyo mara - sani hili Saa haya Maani wa na na yale

Maoni kama bave sana ya daada ye yote wote huu mkuu mkuu bave yo ma wote huu baa na Dawa wana yote ya Baaday yo siku - yote saa bave saa. huu wote na saan Saabana. banali wote huu bava. an wewe kama nakoni huu na huu sani yote sano daady na wote huu sana Saan Kwa na saa huu daay an kama witu ukoma yote hu kwato sana wana bove witu huu mkuu huu auuna kama Baadayo bani mara hali wote sana Kama huu ya kama Saa na sani ya mkuu huu mguu bave weto witu sano we yana. yote huu chu kamo sano witu - baady wewe na mkuu haya Sasa witu mimi wao bave kama sana daadyu sana sana sini kwa mote saa na daady kote bay hand kama huu mku saa bave wito kamna hii wote kama

Sana kamo hay huu mkau kama mguu bave wte wuna Kama kwa baadya sana witu kwa huu sana hale huu haya mwu hote kama yote mimi wote Saa huu sakuna sabana kwa mkuu na yo bave wa haya sana kwa hana sana bave Saa wa kama witu - yote baady ya kama na wote ya wote kawa huu bave na saa bale hano yo yeto kama yote sana kama

Kama wa bave saa haya Pude huu mkuu saaa maani ni sa witu saan no mkuu bave wote kama hua kama sana mimi wote huu hala. Sana yo bave yeto kwa haad ya Saa



Powered by: www.manyamfranchise.com

Baada ya yote haya wote Sana Kama wtu saa Kama na Maani Kama wote bave Kwa saa bave wtu Kwa ya. Sani yalo.

Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kuwasiliana. Ametumia maneno ya Kiswahili ambayo, licha ya kutoeleweka, hayajaunganishwa kimantiki kuunda sentensi zenye maana. Kuna matumizi ya maneno kama vile: **bave, daada ya**, n.k ambayo kwa kweli hayajulikani ni ya lugha gani. Kazi yake imekosa uakifishaji ufaao. Kadhalika, mtahiniwa huyu ameshindwa kujibu swali alilopewa kutokana na udhaifu wake wa kimawasiliano. Ingawa kazi imepangwa ki-aya mambo asemayo katika aya moja hayaelekei kuhusiana na ya aya ya awali. Mtahiniwa wa aina hii kwa kawaida hupata bakshishi tu.

Alama iliyotuzwa: **01**

**Mtungo wa Pili**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...

CHANDA CHEMA UFIKWA PETE

Machozi ya furaha yalinitirika. Sikutaraj haya Kwamba nikieleleza Kutoka Shule Msingi. Walipakuwa. Wanafunzi Wazazi Wangu Walinituza na Kumsahitie Kueleke Vitu aina Mbalimbai. Katika haya nikien lea na masomo Kuanzia darasa la Ku nza mbako tugamilie darasa la nane.

Katika Kiwango cha nane nikendele na masomo. Mwalimu wetu alisungumsa na aliya masomo lakini Kila baada ya Siku Moja Walimu Kutaka Shule yet ya jamii Wanafunzi wote Walinitanasa mtihani Kila baada ya Siku moja. Wanafunzi wote Walipita Sawasawa



Powered by: www.manyamfranchise.com

Ilipotimalisa haya mimi nilikuwa wanafunzi mmoja katika shule ya Sikuamini kwasababu ya mtihani. Machozi ya furaha yalinitoka. Walimu wote ya shule yeto walifurahi sana kama chanda na pete na hata na wanafunzi yote ya shule ya jamii.

Walipatueicikea na walimu zangu katika shule yetu. Walipotoa matokeo kutakana na walimu ni mahombi walipotese kwenda nyumbani nilienda kwa furaha. Walipofika karibu nyumbani wetu nilibatana na wanafunzi mmojo mtipo wasalamia nilienda kwenda mbagi nyumbani wetu.

Banda ya kutika nyumba wazazi wangu walikumkatikisho hapo ndani wazazi walifuraha sana mimi nilipo mwamb nimefahulu kwa mtihani wazazi wangu walifuraha sana.

Mtahiniwa huyu ametumia msamiati wa Kiswahili.Hata hivyo mtindo wake wa kujieleza ni hafifu mno japo ana ufahamu kiasi wa anachosimulia. Insha hii imesheheni makosa mengi ya sarufi na hijai. Kwa mfano: **wanafunzi yote** badala ya **wanafunzi wote, walimu zangu** badala ya **walimu wangu, Wanafunzi yule** badala ya **wanafunzi wale n.k.**Makosa mengi ya hijai yanatokana na athari za lugha ya mama.Mathalani:

a) **Kumsahitie** badala ya **kumsaidia**
b) **Alizungumsa** badala ya **alizungumza**
c) **Wasalamia** badala ya **wasalimia**
d) **Nilipomalisa** badala ya **nilipomaliza**
e) **Nilibatana** badala ya **nilipatana**
f) **Mbako** badala ya **mpaka**



Powered by: www.manyamfranchise.com

Makosa mengine ya hijai ni kama vile **kwasababu badala ya kwa sababu.**
Mtahiniwa huyu ametumia msamiati hafifu mno.Baadhi walekea kuwa unatokana na lugha ya mama.

Kwa mfano:

a) **Tugamilie** (halijulikani ni neno gani)
b) **kiwango** badala ya **darasa** au **daraja**
c) walinifurahia sana **kama chanda na pete.**Tunasema kupendana kama chanda na pete wala si kufurahia kama chanda na pete,.

Uakifishaji wake mbaya mno unaishia kuvuruga muwala wa utungo wake

Alama iliyotuzwa: **05**

**Kundi la Pili (alama 11 – 20)**

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza/kusimulia kwa sentensi/kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa **alama 11-14** huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo.Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/ lugha za mama.

Wanaotuzwa alama **16-20** huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi hutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.


Powered by: www.manyamfranchise.com

**Mtungo wa Tatu**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...

Ilikuwa ni bukrala njema nyuni wa angani walisikika wakiimba nyimbo zao mufti ugedhani ni mvua ya masika. Ambapo nilikuwa nimefanya mtihani wangu wa mock. Nilikuwa nimipata maki ya juu.

Ambapo nilikuwa na furaha mpwitompwi mwilini mwangu. Nilikuwa furaha za kumfanya Shetani haumbiri neno la mterehemezi. Nilifika nyumbani mkambia mama yangu alipatwa na kuruka kama anapepea juu. Akaniambia hata ununua kila kitu chote ninaitaji make nikuwa nayo kama sayansi nilikuwa na sabini na nane akifuatwa na hesabu ambayo nilikuwa na themanini ikifuatwa na kiswahili nilikuwa na sabini kingereza sabini na moja somo la jamii ambamo nayo nikuwa na themanini na mbili. Ndipo nilikuwa na machozi ya furaha yakinitiririka.

Baada ya siku mbili tatu hivi ikawiko siku ya soko ambapo mama alienda kuninunulie zawadi. Akiwa anajiisi mzima kama chuma cha pua. Alipatwa na furaha ya kumfanya haone maji yakitiririka katika kisima cha giningi wakati wa kiangazi mahana



Powered by: www.manyamfranchise.com

alienda akanilafutia sere zuri za shule ambazo ziliaifanya mone kama mimi ni mkubwa kuliko wote.

Punde si punde baba akapingiwa mawasiliano na kufika nyumbani. Nilimweleza vile mlivyo fanga nage akapatwa na furaha telelele akaniambia hataninunua baskeri ya kwenda nayo shuleni alinienge furaha zingine kama za mpwa yaani kechakocho nikajihisi nikomzima. Baba yangu aliniambia nikimaliza mtihani wangu wa K.C.P.E tutaenda uko Amereca akahone mazuri. kutoka hiyo siku nilikua kwa hamani mpaka ikafika siku ya leo ninafanya mtihani wangu wa mwisho nikijua nitapita kwa hamu na ghamu na tutaweza kufika huko America inche zuri.

Sasa ni baada ya miezi tatu ambapo nilipengea babangu mawasiliano akamambia baada ya mtihani tu. tutaweza kwauba huko. Nilikuwa ninaomba mungu wangu nione nikifika huko America

Mtahiniwa huyu anaonyesha kuielewa mada.Hata hivyo utungo wake umejaa makosa ya sarufi na hijai ambayo yanaufanya mtindo wake wa kusimulia kuwa hafifu. Mtahiniwa ana athari za lugha ya mama. Kwa mfano anatumia neno **:hamani** badala ya **amani .** Makosa ya kisarufi yanayojitokeza ni kama vile:

a) ambapo nilikuwa…
b) miezi tatu
c) furaha za
d) furaha zingine…

Makosa mengi ya kitahajia yanatokana na kuhamisha sheria za lugha ya kwanza hadi lugha ya Kiswahili. Tazama mifano:


Powered by: www.manyamfranchise.com

a) **Haumbiri** badala ya **ahubiri**
b) **Nunuria** badala ya **nunulia**
c) **Ninaitaji** badala ya **ninahitaji**
d) **Ikavika** badala ya **ikafika**
e) **Kizima** badala ya **kisima**

Alama iliyotuzwa: **10**

**Mtungo wa Nne**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...

MUNGU HAMWACHII MJA WAKE

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikuyatarajia haya. Ilikuwa likizo wa muhula wa tatu na Januari ilikuwa inanusia wakati wa kwenda shule. Abu yangu hakuwa na hela za kueza kunisomesha hadi kidato cha nne. Mara tu nikaende shuleni mwetu kuona matokeo ya mtihani ambao tulikuwa tumefanya. Nilipofika nilipata matokeo yamebandikwa kwenye ukuta wa afisi. Nilipokaribia hapo afisini moyo wangu ulifurahi, nami sikujua nita pasi.

Nilifika pale palipokuwa matokeo yamebandikwa nikatazama alama zangu za mtihani nilipigwa na butwaa chakari sikuyasadiki macho yangu. Nilirudi nyumbani nikiwa na furaha na bashasha, babangu naye alifurahi kama kibogoyo aliyeota magego. Baba hakuwa anaweza kunisomesha. Kwa kweli Mungu hawatupi waja wake.


Powered by: www.manyamfranchise.com

Niliona gari jipya jeupe likija nyumbani kwetu nilipigwa na butwa chakari. Walikuja hadi mlangoni kwetu, walishuka na kutembea aste aste yaani guu moja guu pili. Waliniamkua "hujambo kijana" niliwajibu "sijambo," "wapi wazazi wako?" wazazi wamwenda gulioni kununua chakula.

Muda mchache tu baba aliingia nyumbani akawakuta hao watu akawasalimu. Wakamwambia babangu tumekuja kumtafuta huyu gulamu kwamba yeye ndiye amepita kwa alama za juu mia tatu sabini na sita. Nilipigwa na butwaa. Mimi ndimi? Mnakuja kunichukua ili niendelee na elimu asante.

Niliingia ndani ya gari hilo nikapelekwa hadi kwenye kituo chao cha WATOTO SOMENI nikafunyiwa kila kitu nikawa tayari kwenda shule. Nikapelekwa hadi shule ya wapendendwa kidato cha kwanza. Nilisoma kidato cha kwanza bila shida yoyote. Muhula wa kwanza sikufukuzwa nyumbani karo ya shule. Maisha huko ilikuwa ya hali ya juu, televisheni ilikuwa na tarakilishi, kila wikendi tulikuwa tukitazama televisheni

Mwaka ulipokua unaelekea mwisho tulifanya mitihani basi ndipo tukafunga shule, niliporudi nyumbani nilipata alama ya A. Baba alinisifu nitie fora masomoni mwangu, wahenga hawakukosea walipo sema mtaka cha mvunguni sharti ainame. Mwaka ulipoanza nilirudi shuleni kusoma


Powered by: www.manyamfranchise.com

kwa bidii kama mchwa wanaojenga kichuguu. Nilisoma hadi kidato cha nne sijawahi fukuzwa karo ila mimi mwenye ndiye sina haja ya kutumia pesa zangu za mfukoni, nilifurahi kama tasa aliyejifungua mapacha.

Mtahiniwa huyu amebainisha kuimarika zaidi.Anaitumia lugha kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wa awali. Ameilewa mada na kuisimulia kwa mtindo wa kiwango wastani. Hata hivyo, hajaikuza mada ipasavyo. Kadhalika ana makosa mengi ya hijai. kama vile:

a) **Kueza** badala ya **kuweza**
b) **Nikaende** badala ya **nikaenda**
c) **Butw**a badala ya **butwaa**
d) **Ulipokua** badala ya **ulipokuwa**
e) **Nita pasi** badala ya **nitapasi**

Utungo huu pia umekosa uakifishaji ufaao ambao unavuruga muwala na muumano wa mawazo. Kwa mfano amekosa kutumia alama za mtajo zinapohitajika. Ametumia koma mahali ambapo angetumia nukta. Kuna makosa ya sarufi kama vile:

a) **Likizo wa** badala ya **likizo ya**
b) Kuchanganya njeo, kwa mfano katika aya ya mwisho
c) Ukosefu wa upatanisho wa kisarufi : Maisha **ilikuwa** ya hali ya juu badala ya maisha **yalikuwa** ya hali ya juu.

Alama iliyotuzwa: **20**

**Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)**

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama **21-25** huwa na ubunifu wa kima cha wastani.Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia kwa makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo mtahiniwa huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama **26-30** huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu.Hata hivyo,insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.


Powered by: www.manyamfranchise.com

**Mtungo wa Tano**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...

Kwa kuwa ni nilikuwa mkia katika darasa letu. Niwakumbatia wazazi wangu kwa furaha. Hapo mbeleni, nilikuwa nikipiga deki. Kaka na binamu yangu wali wakitazama televisheni. "Maina! Maina! Maina! Lo! Wewe ndiye mhasi bora inchini," punde nilisikia. Niliende shuleni kuku nikidanadana kama mpira wa kandanda. Hapo ndipo nilikumbuka methali isemayo, "Usicheke kilema ikiwa uzazi bado uzazi upo."

Nilikumbuka ambavyo walimu wa shule yetu walivyokuwa wananita. Walikuwa wananidharau sana. Walikuwa wakithani kuwa nilikuwa bure bilashi. Nilikuwa nikiomba Mwenyezi Mungu anisaidie niweze kuwashinda wengi waliokuwa wakithani singefaulu katika mtihani wangu. Kaka na binamu yangu walikuwa wamemaka kwa sababu walikuwa wanathani kwamba nitaruka juu na chini kwa furaha. Lakini wapi? Yote hayakuwa.

Punde si punde wanahabari waliwasili. Nilikuwa nimesimama na kubugaa. Sikuyaamini macho yangu. Nilishangilia kwa furaha na kumsifu Mungu kwa nyimbo tamu. "Uwapi? Uwapi? Mbingwa wetu Wanjiru Samuel Maina," wanahabari walitana. Nilitoka nyumbani nisakata densi. Walianza kunitafuta. Nilianza kubabaika. Sikuweza kusema kitu.

Muda si muda mama yangu aliwadia kwa furaha tele. Nimweleza yote yaliyojiri hapo awali akiniashukuru Mola ku vitendo vyake vya huruma. Kwani, Mola hamwachi mja wake. Wanahabari wanipa muda mdogo wakisherehekea



Powered by: www.manyamfranchise.com

watu wa ukoo wetu. Adhuhuri ilipofika niliamua kwenda katika vyombo vya habari ili kuhojiwa. Nilipofika huko, wanahabari walianza kuniuliza nilichokifanya ili kupita mtihani. Niliwaeleza hadithi yangu ilivyokuwa. Walistaajabu kwa kutoamini niliyosema. Niliwapea siri zangu ambazo zilifanya nipite mtihani. La tatu walinihimiza niwape motisha wanafunzi wengine ichini. Niliwapa makali na kuwahimiza wasome kwa bidii ya mchwa anaye jenga kichuguu.

Niliporudi nyumbani, Mama alikuwa ameandaa chakula kitamu kama asali. Hapo ndipo nilielewa dhahiri shahiri kwamba mcheza kwao hutunzwa na chanda chema huvishwa pete. Pia ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firaoni, Shangazi yangu alipea baiskeli na bunda la noti. Sote tuliende sebuleni na tukala chamcha. Nilipomaliza kula niliele kea shuleni mwetu ili kuhakikisha kuwa niliyoona yalikuwa ya kweli.

Nilipofika shuleni wanafunzi wote walikuwa vinywa wazi. Walikuwa wakiniangalia kama sanamu ya Mzee Jomo Kenyatta. Nilipofika majilisi nilimkuta mwalimu wetu wa darasa. Wote walinichukuwa juu na wakaanza kuimba, Mbigwa wetu! Mbingwa wetu! Wote walishangilia kwa furaha.

Nilirudi nyumbani na kumshukuru Mola kwa kunifanyia wema kama huo. Siku zilipopita wasichana walianza kuniulia. kiw

Mtahiniwa huyu amedhihirisha kuwa ameilewa mada na kuisimulia kwa mtindo mpevu na kwa mvuto zaidi akilinganishwa na wa awali.Huyu ana makosa machache ya kimtindo akilinganishwa na wa awali. Hata hivyo insha hii bado ina makosa ya kihijai, kisarufi,na msamiati..Mifano ya makosa ya hijai ni kama vile:


Powered by: www.manyamfranchise.com

a) **Inchini** badala ya **nchini**
b) **Niwakumbatia** badala ya **niliwakumbatia**
c) **Walithania** badala ya **walidhania**
d) **Waliwasiri** badala ya **waliwasili**
e) **Anayenjenga** badala ya anayejenga
f) **Nisakata** badala ya **nilisakata**
g) **Nili anza** badala ya **nilianza**, n.k

Baadhi ya makosa ya hijai yanatokana na athari za lugha za mama.
Makosa ya sarufi ni kama vile **nilioyeona, yaliyojiri hapo awali akimshukuru, niliwapea** n.k

Kadhalika kuna makosa ya msamiati kama vile:
a) Mhasihiwa badala ya **mtahiniwa**
b) **Usicheke kilema ikiwa uzazi bado ungalipo-** imetundikwa tu
c) **Bure bilashi** badala ya **sikuyamudu masomo**

Alama iliyotuzwa: **23**

**Mtungo wa Sita**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:
Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...

MCHEZO WA KUKATA NA SHOKA

Machozi ya furaha yalinitiririka Sikutarajia haya. Ilikuwa yaumu ambayo nitakuwa nikikumbuka aushini yangu. Siku yenyewe ilikuwa siku ya michezo katika shule yetu. Shule yetu ingecheza dhidi ya shule jirani. Mnamo mwendo wa asubuhi na mapema watu wa tabaka mbali-mbali walikusanyika kweli kweli. Kila upande isi mashariki, si Maghribi, si kusini na wala si kaskasini kote kilijazwa na waja anuwai.

Siku hiyo mimi na rafiki yangu wa dhati tulikuwa na wasiwasi mwingi kwani shule ya jirani walikuwa gwiji na stadi katika upande wa michezo Dakika chache


Powered by: www.manyamfranchise.com

baada ya maandalizi kumalizika wachezaji ajmaina waliyitomo kwenye uga huko Ikionekana liwakiwa na iwasiwasi mwasi kando.

Hayawi hayawi huwa kila mchezaji alichukua nafasi na kuanza kuomba mungu kwani mwomba mungu si mtovu. prr! prr! kipenga kilipulizwa na kila timu ilianza kuonyesho umahiri wake wa kusakata mchezo. wakati kila mmoja wetu alikuwa na furaha ribariba kwani mwia kiduchu wachezaji wa timu yetu walianza kutoa pasi fupi fupi. ungedhani walikuwa na spaki wa kujinasua mpira mvutuni mwa wapinzani wa timu walianza kutiwa waha na ilikuwa waziwazi kwamba wangefunzu thali kusaka michezo.

punde si punde mashabulizi ya paka ilianzo na mchezaji wa kiungo cha kati alianza kupiga chenga kwa wacheza watu na kupika mpira kwa ufundu wa juu sana. mlindalango wa timu geni aliruka upande wa kushoto huku mpira ikitimia kimiani upande wa kulia.

Mwia kichele kipenga cha mapa bazuko kilipulizwa. wachezaji wote walitoka sowia ili wapate nafasi kidogo cha kupat mashauri kwa kochi yao. kwani jungu kuu halikosi ukoko. Dakika chache baada kipenga cha kwaheri ya kuona kilipuli


Powered by: www.manyamfranchise.com

Mchezo ulianziko kwa mara ya pili. Wapinzani wetu walionekana wametia fora lakini walibezwa na kufungwa huku wakikumbushwo jogoo hawiki ugenini. Kochi yao alikuwa akitembeatembea lakini juhudi zake hazikufdafu. Walifungwa kwa bao tano kwa nunge. Kweli ilikuwa mchezo wa aina yake na mpaka sasa naikumbuka kana ilikuwa dakika chache. Inna, asiyekubali kushindwa si mshindani.

Mtahiniwa huyu amebainisha ukomavu zaidi akilinganishwa na wa awali.Ameielewa mada na kuisimulia kwa mtindo mzuri wenye mvuto kiasi.Amebainisha wepesi wa kuitumia lugha kusimulia kisa chake. Ametumia mbinu mbalimbali za kimtindo kama vile tabaini: si mashariki; si magharibi.., na methali. Hati yake ni nadhifu na inasomeka.Insha ina makosa machache ya sarufi na hijai.

Makosa ya sarufi ni kama vile;

a) **Tabaka mbalimbali** badala ya **matabaka mbalimbali**
b) **Mchezo ilianziko** badala ya **mchezo ulianza**
c) **Kochi yao** badala ya **kochi wao**
d) **Mashabulizi ya paka ilianza** badala ya **mashambulizi ya paka yalianza.**
e) **Ilikuwa** mchezo badala ya **ulikuwa mchezo**

Makosa ya hijai ni kama vile:

a) **Mashabulizi** badala ya **mashambulizi**
b) **Kupika** badala ya **kupiga**
c) **Mapabazuko** badala ya **mapambazuko**

Alama iliyotuzwa: **29**

**Kundi la Nne (Alama 31 – 40)**

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala/masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama **31-35** huitumia lugha kwa wepesi zaidi. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama **36-40** huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu zaidi na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi au mitindo mbalimbali ya kujieleza ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi au mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.



Powered by: www.manyamfranchise.com

**Mtungo wa Saba**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

KASKI ISIYOGHAFILIKA

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...niliyokuwa nimeyasikia kwenye televisheni. Skulini nilikuwa kila mara nikishika mkia ilhali nilikuwa nimeibuka mshindi katika mtihani wa astashahada. Nilidhani ya kwamba ilikuwa ni ndoto lakini mwishowe nilikuja kusadiki. Wavyele wangu walijawa na furaha mpwito mpwito mithili ya mja aliyeshinda katika mchezo wa yalau yalamu.

Kwa hakika ndoto yangu ya kuibuka mshindi katika mtihani ilikuwa imetimia. Tangu nianze darasa la chekechea sikuwa nimewahi kuibuka mshindi katika mtihani wowote ule nilikuwa nikishika mkia. Waja walianza kumiminika kwetu. Uwanja wetu ukajaa sisisi hadi kukawatapika wengine nje. Si kwa sababu uwanja wetu ulikuwa mdogo, ulikuwa mkubwa kama bahari.

Walimu wa shule yetu ya Johari na watahiniwa wenzangu pia walikuja kwetu kusherehekea ushindi wangu. Wale waliokuwa wakinicheka walikuwa wakilia na kusaga meno kwa sababu walikuwa wamefeli katika mtihani wao wa astashahada na sasa hawangeweza kuendelea na masomo. Wengine wao walibaki wameduwaa waa na kubung'aa


Powered by: www.manyamfranchise.com

ngāa. Wengine walikuja kuniomba msamaha kwa uovu waliokuwa wamenitendea.

Nilihojiwa na vikundi vya magazeti anuwai na waja wa vipindi mbalimbali vya televisheni. Nilikuwa na bashasha nyingi sana na kwa hivyo sikuweza kuzungumza maneno mengi. Jamaa zangu wa mbali walijitahidi kadiri ya uwezo wao kuja kusherehekea nami. Nilipomaliza kuhojiwa vikundi vya mageti viliendа kisha wavyele wangu wakaandaa sherehe ya kufana.

Baiti yetu ilipambwa ikapambika kwa maua kochokocho. Ungedhani ya kwamba kulikuwa na mombasa kwamеremeta ya kufana nyumbani kwetu. Vyakula vingi vilipikwa vikapikika. Waja walikula shibe yao huku nyimbo za kumtukuza Jalali zikisikika.

Tulipokuwa tukitazama runinga tukiwa sherehеni nilijawa na furaha riboribo mithili ya kibogoyo aliyeota magego na segego meupe pepepe katika shamra shamra za dhifa ya nyama choma kujiona kwenye runinga. Sherehe ilipoisha kila mmoja alienda maskanini mwake huku wavyele wangu na mimi tukibaki kupata


Powered by: www.manyamfranchise.com

ubwabwa wa mwana mtamu. Sitawahi kuisahau yaumu hiyo katika aushi yangu.

Mtahiniwa huyu ameilewa mada ila hajaikuza vyema ipasavyo.. Anajieleza kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wale wa vitengo vya chini. Ametumia tamathali za usemi kama vile tashbihi **mithili ya mja**… , n.k majazi-**Johari -** Hati yake ni nadhifu na inasomeka kwa urahisi.Hata hivyo uteuzi wa kichocheo cha furaha yake waalekea kuupweza ubunifu wake. Anatusawiria picha ya mhusika asiyefanya bidii kisha kufanikiwa kimiujiza.Yumkini kisa chake kingekuwa na upekee na mvuto zaidi iwapo angemsawiri mhusika aliyekumbwa na matatizo kisha akafauilu kutokana na jitihada yake, au mtahiniwa aliyefaulu vyema katika mtihani mgunu kutokana na bidii yake.

Insha hii ina makosa machache mno ya sarufi na hijai.Makosa ya sarufi yaelekea kuwa ya kimuundo kama vile: **ungedhani ya kwamba kulikuwa na Mombasa kwamereremeta** …, **wavyele wangu na mimi(** huu ni muundo wa Kiingereza).

Alama iliyotuzwa: **32**

**Mtungo wa Nane**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

BIDII HULETA FANAKA

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha inayoanza kwa maneno yafuatayo:

Machozi ya furaha yalinitiririka. Sikutarajia haya ...
Kwani mtihani wa mwaka huo ulikuwa mgumu ajabu. Nilikuwa nimeufanya mtihani huo kwa ujasiri ila sikutarajia kuwa ningezoa alama hizo. Nilikuwa nimezoa alama mia nne na ishirini. Moyo wangu ulijawa na furaha sufufu kama kibogoyo aliyeota magego na sagego katika shamrashamra za kula nyama choma.

Majirani na jamaa waliingia mmoja baada ya mwingine kuja kunipongeza. Nilimshukuru Rabuka kwa kunitunukia alama zile. Nilikuwa mwanafunzi bora nchini kote. Abu na nina walikuwa wamejawa na furaha kama mvuvi



Powered by: www.manyamfranchise.com

aliyekinasa kishazi cha samaki. Moyoni nilimshukuru nina kwa kunipa usia kila mara kuwa nisikate tamaa masomoni.

Baada ya majirani na jamaa kuondoka nilikaa chini ili nifikirie jinsi nilivyozoa alama hizo. Ghafla bin vuu nilikuwa nimetumbukia katika bahari la mawazo na kumbukumbu. Nilikumbuka jinsi nilivyotia bidii za mchwa ajengaye kichuguu ili niweze kufaulu maishani. Sikusahau usia wa wavyele wangu kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha. Nilitambua kuwa nilikuwa na bahati kama mwana aliyezaliwa ijumaa. Nilijua kuwa bidii na kujitolea kwangu kulizaa matunda. Hapo ndipo nikatafakari methali ya akina babu kuwa mchumia juani hulia kivulini.

Kabla ya nukta kusadifu na kuwa dakika nilisikia sauti za akina mama zikiimba kwa sauti nyororo. Nilipotazama sikuamini niliyoyaona. Nyuma yao kulikuwa na wasomaji habari. Walinijia kwa mbio za swara na kuniuliza maswali machache. "Mimi ningependa kuwatia shime watahiniwa wa mwaka ujao. Tieni bidii masomoni ili mushughulikie maisha yenu ya baadaye. Kumbukeni kuwa nyinyi ndio serikali ya kesho. Bidii, kujiamini na kujitolea ni vitu vitatu vitakavyokusaidia." Niliwajibu.


Powered by: www.manyamfranchise.com

Baada ya hayo wote waliondoka na kwenda zao. Kabla ya nzi kufa kidondani, mbunge wa eneo letu aliwasili. Alinipongeza na kunituza kwa vitabu vya shule ya upili. Furaha sufufu ilinitinga moyoni si haba. Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kuonana na mbunge huyo. Nilimshukuru Kudusi kwa kunifikisha kiwango kile.

Hata hivyo hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Kunao walinionea gere lakini nikawapuuza na kujua ni bidii yangu iliyonifikisha hapo. Hakuna chochote wangefanya kwani Mola akikutunukia binadamu hawezi kukutunukua. Ilitaki tu wajiambie kuwa waache yaliyopita na wagange yajayo.

Kwa kweli nilimshukuru Mterehemezi kwa zawadi ile. Sasa nilielewa barabara kuwa bidii yako 'ngao yako. Moyoni nilijawa na furaha na buraha huku kijiji chote kikinipongeza kwa shangwe na nderemo.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuikuza vyema na kwa ukomavu zaidi kimaudhui na kifani.Tofauti na watangulizi wake, ameiunga hali yake ya sasa na ya awali kwa kubainisha sababu ya kutotarajia fanaka yake .Uteuzi wake wa mtindo unaipa insha yake shani ikilinganishwa na za awali.Anatumia vipengele vya kimuundo kama vile mbinu rejeshi na dayolojia za wahusika kwa ufanifu bila kuvuruga muwala na muumano wa mawazo yake.Mawazo yanatiririshwa kimantiki bila kukatizwa kwa uchopekaji wa msamiati ambao ulibainika katika insha za vitengo vya chini.

Kwa jumla hii ni insha ambayo ina uasilia na inaweza kuaminika kuwa ubunifu asilia wa mtahiniwa wa kiwango hiki. Makosa ya kisarufi yanayobainika ni kama vile: kosa la uakifishaji-**ijumaa** badala ya **Ijumaa,** na kosa la urejeshi-**walinionea** badala ya **walionionea.**

Alama iliyotuzwa: **36**


Powered by: www.manyamfranchise.com

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano msamiati wa magonjwa unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu magonjwa.Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri au kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali (ngazi/viwango) tofautitofauti za maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza/mitindo ya usimulizi..

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waonywe dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake.Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati/matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa.Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa, wasitumie kimoja tu.Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwa kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi. Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo, hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.


Powered by: www.manyamfranchise.com